**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

**MKOA WA GEITA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE.**

---

SHULE YA SEKONDARI BUKOMBE,
S.L.P 58,
**BUKOMBE.**
TAREHE19/04/2024.

NAMBA ZA SIMU:
MAKAMU MKUU WA SHULE: **+255 781 746 228**
MWANDAMIZI TAALUMA: **+255 785 363 343**
MHASIBU: **+255 625 503 265**
MKUU WA SHULE: **+255 763 643 501**
***Email***. bukombesecondary@gmail.com

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………………….
S.L.P……………………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUKOMBE MWAKA 2024.**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **2024** katika tahasusi ya **HGL/HGLi**.
2. Shule ya Sekondari Bukombe ipo umbali wa km **15** kutoka makao makuu ya Wilaya (Ushirombo) katika Kijiji cha Bukombe na ipo umbali wa Km 1 kaskazini mashariki mwa barabara kuu ya lami iendayo Rwanda na Burundi ikitokea (**Dar/Moshi/Mwanza - Kahama –Bukoba).**

   Muhula wa masomo unaanza tarehe **01.07.2024** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **30.06.2024,** mwisho wa kuripoti ni wiki mbili baada ya shule kufunguliwa.

3. **Mambo muhimu ya Kuzingatia:**

   **Sare za Shule:**

   a) Sare ya Shule hii ni suruali ya rangi ya Kijivu nyeupe no.1(crator/istim) isiyo na michirizi yoyote na yenye mifuko miwili (2) pembeni na nyuma mmoja (1). Pia iwe na marinda manne (4), mawili (2) upande wa kulia na mawili (2) upande wa kushoto na ifunike kifundo cha mguu. (**Jozi mbili**)

b) Shati Jeupe tetroni la mikono mifupi (**Jozi mbili**).
c) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi visivyo na urembo wowote.
d) Soksi nyeusi ndefu jozi mbili (2).
e) Mkanda mweusi wa ngozi.
f) **Sare za michezo**; raba za michezo, bukta na tsheti (**rangi nyeupe/blue**) tu isiyo na nembo ya klabu ya mpira.
g) Nguo za kushindia **(Shamba dress)** suruali nyeusi na tshet ya bluu isiyo na mandishi.
h) Tracksuit moja (1) ya rangi ya bluu.
i) Sweta moja (1) rangi ya ugoro lenye mstari mweupe kifuani kutoka kulia kwenda kushoto, linapatikana shuleni.
j) Tai ndefu rangi ya kijivu.
k) Tsheti moja (1) rangi ya kijivu yenye kola nyeusi na nembo ya shule inapatikana shuleni.

**ANGALIZO:**
Nguo tofauti na hizo zilizotajwa hapo juu katika kipengele (a) – (k) hazitakiwi kabisa shuleni.

- **Bima ya Afya**: Hakikisha kijana wako anakuja na Bima ya Afya shuleni kwa ajili ya matibabu. Kama hana Bima ya Afya atalazimika kuja na Tsh**. 51,000/= mkononi** kwa ajili ya kupatiwa Bima ya Afya (NHIF). **BIMA NI LAZIMA. (Fedha hii itapokelewa wakati wa kuripoti shuleni tu.)**

## 4. MICHANGO MBALIMBALI.

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

Michango yote (**isipokua fedha ya Bima ya Afya**) ilipwe kwenye akaunti Na. **32501200039 NMB** jina la akaunti **Bukombe Secondary School.** (***Andika jina kamili la mwanafunzi kwenye Risiti ya malipo ya benki.)***

**NB:** Risiti ya malipo (***Bank pay in slip) ya michango iwasilishwe kwa Mhasibu wa shule siku mwanafunzi anaripoti shuleni***.

5. **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**:

    i. Faili moja (**folder file**)
    ii. Vitabu vya masomo vya tahasusi husika (TIE).
    iii. Ream ya karatasi $A_4$ mbili (2), kila muhula Ream moja (1).
    iv. Jembe lenye mpini, kwanja, panga na ndoo mbili za lita 10.
    v. Squeezer na soft broom.
    vi. Godoro futi $2\,^1/_2$ x 6 na chandarua.
    vii. Mashuka mawili (2) ya rangi ya bluu na blanketi moja.
    viii. Sanduku imara la chuma lenye kufuli.
    ix. Sahani, bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula.
    x. Ndoo moja (lita 20) kwa ajili ya kutunzia maji kwa usafi binafsi.
    xi. Vifaa vingine muhimu mfano: sabuni, mafuta ya kupaka, dawa ya meno, mswaki, madaftari n.k
    xii. Picha (Passport size) 5: 3 za Mwanafunzi na mbili za wazazi/walezi pamoja na namba zao za simu.

**ANGALIZO.**

Fomu zifuatazo zinatakiwa kurudishwa shuleni zikiwa zimejazwa vizuri.

i. Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai, pamoja na kutomiliki simu shuleni
ii. Fomu ya vipimo vya afya ya mwanafunzi (**Vipimo vithibitishwe na Daktari wa Hospitali ya Serikali)**
**iii. Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.**
**iv. Kivuli cha Matokeo ya awali (result slip) kidato cha nne.**
**v. Kivuli cha Cheti cha kutoka shuleni (Leaving Certificate)**

## 6. SHERIA ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978, pia inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Hivyo kwa kipindi chote utakapokuwa mwanafunzi wa shule hii, utatakiwa kushika na kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zote za shule ukiwa ndani na nje ya shule **kwani utakuwa ukiiwakilisha shule popote utakapokuwa. Kutokujua sharia hakutakuwa kinga ya kutokuchukuliwa hatua stahiki**.

### (a) TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE

1. **HESHIMA**:

   Kila mwanafunzi anatakiwa kwanza kujiheshimu mwenyewe, kuwaheshimu walimu,wazazi/walezi,wageni na viongozi kwa ujumla.

2. **USAFI**:

   Kila mwanafunzi anatakiwa kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule kwa ujumla.

3. **RATIBA YA SHULE**:

   Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu ratiba ya shule.Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mazingira ya shule bila ruhusa maalum kutoka kwa uongozi wa shule. Aidha mwanafunzi anatakiwa kuwahi darasani na katika shughuli mbalimbali za shule ikiwa ni pamoja na kutii wito (**kengele.)**

### (b) MAKOSA YA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI.

1. Wizi wa aina yoyote.
2. Uasherati, ushoga na ubakaji
3. Utumiaji wa vilevi na dawa za kulevya (mirungi, kuber,bangi, sigara n.k)
4. Kupiga/kupigana/kutoa lugha chafu kwa wanafunzi, walimu au jamii.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6. Kudharau bendera ya Taifa,nembo ya Taifa, fedha na picha za viongozi.
7. Kusababisha / kubeba/kutoa mimba.
8. Kugoma,kuchochea/kuongoza mgomo na kuvuruga amani na usalama shuleni /jamii.
9. **Mwanafunzi kumiliki line/simu ya mkononi na viambata vya simu.**
10. Udanganyifu wa aina yoyote katika mitihani.
11. Kugomea adhabu yoyote halali.
12. Kutotii serikali iliyopo madarakani na chama tawala.
13. Kuwa nje ya shule bila sare ya shule na bila ruhusa/kibali maalum kutoka kwa uongozi wa shule.

14. Kuonekana kwenye nyumba za wageni na kumbi za starehe.
15. Utoro/kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini bila taarifa.
16. Kuoa au kuolewa.


**ANGALIZO:** ***Mwanafunzi atakayebainika/kukamatwa nje ya eneo la shule bila sare ya shule na ruhusa kutoka kwa uongozi wa shule atatozwa tofali 100 za saruji zitakazokabidhiwa shuleni.***

## (c) MAKOSA YAFUATAYO YAKIJIRUDIA YATASABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Utoro wa aina yoyote.
2. Kuchelewa kufika shuleni (baada ya likizo) na katika shughuli mbalimbali za shule.
3. Kutokuvaa sare rasmi ya shule kulingana na ratiba ya shule
4. Uchafu wa mwili (kutokunyoa ndevu/nywele,kutokuoga n.k ) na kutokutunza mazingira ya shule

**TANBIHI**: Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vifaa vya umeme kama vile pasi,heater,n.k. Aidha mwanafunzi haruhusiwi kumiliki redio yenye kubeba memory card/flash**.**

**KARIBU**



# FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

***(To be completed by a medical officer in respect of all form one/form five Entrants)***

Full names ……………………………………………………………………………………

Age ………………………………………………… Sex ……………………………………

Blood count (Red and White) ……………………………………………………………

Stool Examination …………………………………………………………………………

Urine analysis ……………………………………………………………………………

Syphilis Test ………………………………………………………………………………

T.B Test ……………………………………………………………………………………

Eye Test ……………………………………………………………………………………

Ears …………………………………………………………………………………………

Chest ………………………………………………………………………………………

Spleens ……………………………………………………………………………………

Abdomen ……………………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION**: E.g. Physical defects or impairments, Infections chronic of family diseases etc.

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………

I certify that the above is fit/unfit to pursue as stated above.

Signature ……………………………

Designation …………………………

Date …………………………………

**NOTE**: Medical officer: At time of examination please treat the Individual for any aliments you note.

**N.B**: This completed form should be sent to the school with your acceptances form or brought when you come to the school. No one will be enrolled without a certificate of physical fitness.

MKUU WA SHULE
BUKOMBE SHULE YA SEKONDARI

**FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.**

## A: HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi.................................................................... Tarehe ya kuzaliwa.......................................

   Umri........................ Kabila.............................................
2. Shule aliyotoka .................................................... Mkoa.................................... Wilaya................................
3. Jina la Baba/Mlezi.................................................................... Kazi yake.......................................................

   Anakoishi........................................................... Namba ya simu................................................................
4. Jina la Mama/Mlezi.................................................................. Kazi yake........................................................

   Anakoishi........................................................... Namba ya simu..................................................................
5. Dini.........................................................................

## B: MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

Mimi................................................................................ Mtoto wa................................................................ Kutoka Wilaya ya.................................................... Nafunga mkataba huu na kuahidi kwamba sitashiriki katika fujo/mgomo wowote na sitafanya kosa lolote la jinai nikiwa mwanafunzi wa shule ya sekondari Bukombe.

Ninakubali pia kwamba endapo nitafanya mambo yaliyo kinyume na Mkataba huu, hatua z kinidhamu na kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Jina la mwanafunzi..................................................................... Saini................................................ Tarehe .......................
Jina la Mzazi/Mlezi.................................................................... Saini................................................ Tarehe.........................

## C: FOMU YA MZAZI/MLEZI YA KUKUBALI SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Mimi .............................................................................. Mzazi/Mlezi wa ......................................................................wa Kidato cha .................................... Mwaka...................................... Ninakubali kuwa mtoto wangu atahudhuria masomo na kuzingatia sheria zilizowekwa kuanzia sasa hadi atakapomaliza kidato cha .............................. Mwaka........................ katika shule ya sekondari Bukombe.

Aidha ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule ikiwemo sare za shule na mahitaji mengine yaliyoainishwa na shule. Hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu endapo nitashindwa kumpatia mahitaji ya shule mtoto wangu.

Saini ya Mzazi/Mlezi ..............................................................................
Tarehe ............................................................................

MKUU WA SHULE
BUKOMBE SHULE YA SEKONDARI

7. KUHUSU MWANAFUNZI KUMILIKI SIMU SHULENI.

Kikao cha bodi ya shule cha tarehe 17.08.2017 kilikubaliana na adhabu zifuatazo kwa mwanafunzi atakae kamatwa na simu shuleni:-

1. Kuchapwa viboko vine (4) mbele ya wanafunzi wote mstarini.
2. Kusimamishwa masomo siku 21.
3. Siku ya kurudi shuleni mwanafunzi atatakiwa kuja na mzazi/mlezi wake na faini ya shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=)
4. Simu na kadi ya simu vitavunjwa mbele ya wanafunzi na mzazi/mlezi.

N.B Endapo mzazi/mlezi atashindwa kutekeleza vipengele tajwa (1 – 4) mwanafunzi atafukuzwa shule.

JINA LA MWANAFUNZI.............................................................. JINA LA MZAZI...........................................................
SAHIHI: ............................................ SAHIHI...........................................
TAREHE: ...................................... TAREHE......................................

8. KUHUSU MWANAFUNZI KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE BILA SARE YA SHULE NA RUHUSA.

Kikao cha bodi ya shule cha tarehe 17.04.2024 kilikubaliana na adhabu zifuatazo kwa mwanafunzi atakaye kamatwa nje ya mipaka ya shule bila sare ya shule na ruhusa:-

1. Kuchapwa viboko vine (4) mbele ya wanafunzi wote mstarini.
2. Kusimamishwa masomo siku 21.
3. Siku ya kurudi shuleni mwanafunzi atatakiwa kuja na mzazi/mlezi wake na kukabidhi tofali 100 za saruji.

N.B Endapo mzazi/mlezi atashindwa kutekeleza vipengele tajwa (1 – 3) mwanafunzi atafukuzwa shule.

JINA LA MWANAFUNZI.............................................................. JINA LA MZAZI...........................................................
SAHIHI: ............................................ SAHIHI...........................................
TAREHE: ...................................... TAREHE......................................

MKUU WA SHULE
DOKOMBE SHULE YA SEKONDARI